SOMO LA NNE



KWA NINI YESU ALIKUFA?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

ALIKUFA KAMA SEHEMU YA MPANGO WA MUNGU

Kufanyia kazi mpango

Waandishi wa Agano Jipya wanatuambia kwamba kifo cha Yesu hakikuwa cha makosa Fulani, isipokuwa sehemu ya mpango na makusudi ya Mungu. Mungu alikuwa akitumia maovu ya watu kama njia ya msamaha kwa wale watakaogeuka na kuziacha dhambi zao. Cha kushangaza, wale waliomsulubisha Yesu wangeupata msamaha huu pia! Matendo yao maovu yalifanya njia ambayo kupitia hiyo hata dhambi *zao* zingesamehewa! Baadaye katika somo hili tutaona *jinsi* kifo cha Yesu kilivyoufanya msamaha kuwezekana.

MUNGU ALIJUA KUWA YESU ANGEUAWA

Mungu aliamua mapema kuwa Yesu alitakiwa kufa. Angalia Matendo 2:23

.....

.....

.....

.....

Mungu ni wa Uweza

MUNGU ALITUMIA CHUKI ZA WATU KATIKA MPANGO WA UUNGU WAKE

Yesu alikuwa mwanga mkuu

Mungu hakuwafanyi watu wamchukie Yesu, bali alitumia chuki iliyokuwa ndani ya mtu kuukamilisha mpango Wake. Utakatifu wa maisha ya Yesu yaliufanya uovu wa wengine kudhibitika zaidi. Hivyo walimchukia Yesu, na wakaona vyema kumuua kuliku kudhihirishwa kwa maisha yao ya dhambi kwa mwang Wake. Yesu alikuwa mwanga katika ulimwengu wa giza. Watu walijaribu kutofautisha mwnga, wakipendelea giza la maisha yao ya dhambi. Angalia Yohana 3:19

.....

.....

.....

.....

MUNGU ALITUMIA CHUKI YA WATU KATIKA MPANGO WAKE WA UUNGU

Kumbukumbu ya kale: Kusulubiwa kulikuwa kwa taratibu na kifo cha maumivu. Mikono ya mhusika na vidole vyake vilipigiliwa misumari msalabani. Yesu aliumizwa vibaya sana kabla ya kusulubiwa.

Pamoja na watu wengi kumchukia Yesu, kulikuwepo na wengine wengi waliovutwa Naye. Kukubalika kwake kuliwaudhi watawala na ilikuwa sababu nyingine ya Kumchukia.[1] 1 Mtawala wa Rumi alijua wamemchukia Yesu, hivyo alitaka Kumfungua. Soma Mathayo 27:17-18. Andika mst. 18

.....

.....

[1] Kulikuwepo na sababu nyingine nyingi zilizomfanya Yesu achukiwe. Angalia Yohana 5:18, Luka 19:45-48.

Kifo cha Yesu hakikuwa ghafla, wala mwisho. Mungu aliwaruhusu watu wafanye uovu ili kupatikana kwa uwezekano mkubwa ulio mzuri, kama waandishi wa Agano Jipya wanavyoelezea katika sehemu inayofuata.

Adhabu

ALIKUFA KAMA ADHABU YA DHAMBI

Mungu ni wa haki. Kama hakimu wa duniani asivyoyapuuzia makosa, na Mungu hatayapuuzia maovu tunayotenda. Hivyo dhambi lazima iadhibiwe, na adhabu ya Mungu kwa ajili ya dhambi ni kifo.[2] Lakini haki ya Yesu siyo kwamba humfanya Awe mhukumu wa haki (Somo la 2 na 3), pia Humfanya *mwakilish*i wa haki. Kwa sababu hana dhambi Mwenyewe, aliweza kuchukua dhambi na adhabu yaw engine.

YESU ALITESEKA KATIKA NAFASI YA WAAMINI

Yesu wa haki na mtakatifu aliteseka kwa ajili ya wasio haki, kuwarudisha kwa Mungu. Angalia 1 Petro 3:18

Mwenye haki kwa wasio haki

.....

.....

.....

.....

Kushindwa kutunza amri za Mungu huleta laana ya Mungu. Yesu alichukua laana hii badala ya kila muumini. Angalia Wagalatia 3:13

.....

.....

Alichukua laana

.....

YESU ALIKUWA MWANAKONDOO WA MUNGU

Kabla Yesu hajaja, wanakondoo na wanyama wengine walitolewa kafara. Dhambi ilisherehekewa kwa kuhamishiwa kwao, na waliuawa. Walikufa kwa nafasi za wengine- wasio na hatia kwa wenye hatia. Hii ilikuwa kivuli cha kile ambacho Yesu alikuja kufanya. Yesu anaitwa Mwanakondoo wa Mungu kwa sababu Alikufa, kama mwanakondoo, kwa nafasi yaw engine. Wanyama hawawezi kuchukua dhambi, lakini kifo cha Yesu huondoa dhambi mara moja tu.[3] Angalia Yohana 1:29



Wanakondoo walitolewa kafara

.....

.....

.....

.....

Wanakondoo pia walitolewa kafara katika Pasaka za Wayahudi. Siku ya sherehe iliheshimiwa pale Mungu alipowaacha (kuvuka) wazaliwa wa kwanza kwa kila nyumba iliyopakwa damu ya mwanakondoo. Mwanakondoo alikufa badala ya mwana. Yesu ni Mwanakondoo wa Pasaka aliyekufa katika nafasi ya kila muumini.[4]

[2] Warumi 6:23.

[3] Waebrania 10:11-12.

[4] 1 Wakorintho 5:7.

ALIKUFA KUWAPATANISHA WAAMINI NA MUNGU

Mafundisho ya Agano Jipya liko wazi – dhambi humchukiza Mungu mtakatifu, hivyo mtu wa hivyo ni adui wa Mungu. Lakini Yesu alikufa badala ya waamini ili kuwapatanisha na Mungu.[5] Siyo tena adui wa Mungu kwa sababu dhambi zao zimeadhibiwa kwa Kristo na kuondolewa.

Uadui dhidi ya Mungu

KIFO CHA YESU HUPATANISHA

Sasa waamini hawa wamewekwa sawasawa mbele za Mungu wanaweza kufurahia. Soma Warumi 5:10-11. Andika mstari 11

.....

.....

.....

HAKUNA LAUMU ILIYOBAKI

Hakuna laumu/lawama zaidi kwa waamini. Mungu ni rafiki zao sasa. Hakuna cha kuogopa kutokana na Siku ya Hukumu. Angalia Warumi 8:1

Urafiki na Mungu

.....

.....

.....

Waamini wa kweli pekee ndio wanaopatanishwa na Mungu. Tutapata kuwa na uelewa wa wazi ni nini maana ya kuamini tutakapofikia somo la 6.

KUPATANISHA KWA GHARAMA

Ilimgarimu Yesu gharama kubwa kuwapatanisha waamini kwa Mungu. Yesu alituambia kwamba kifo Chake kilikuwa "fidia kwa wengi".[6] Fidia ni gharama ya fedha inayolipwa kumrudisha mtu tena. Magaidi/wateka nyara kwa mara nyingi hudai fidia. Yesu alitoa maisha yake sehemu ya wenye dhambi kama fidia kuwaokoa waamini tena kwa Mungu. Waamini hawajitawali tena tangu waliponunuliwa na Yesu, na ni lazima waishi kama Yeye. Angalia 1 Petro 1:18-19

Gharama ya fidia!

.....

.....

.....

.....

.....

ALIKUFA KUFUNGUA MBINGU KWA WAAMINI

Waamini kutoka kila nchi wataingia Mbinguni. Agano Jipya linaielezea Mbingu kama sehemu takatifu ambapo Mungu na malaika Zake wanaishi. Hakuna kichafu au dhambi kinaweza kuiingia.[7] Waamini wanapatanishwa na Mungu kupitia kifo cha Kristo, na dhambi zao zimeondolewa. Hivyo hakuna kinachoweza kuwazuia kuingia Mbinguni watakapokufa.

Mbingu ni kwa rangi zote

[5] Wakolosai 1:20.
[6] Marko 10:45.
[7] Ufunuo 22:15

Maandalizi endelevu

SEHEMU YA AKIBA

Yesu mara kwa mara aliongea juu ya Mbinguni, na Aliwaambia wanafunzi Wake kuwa alikuwa anawatangulia kuandaa sehemu kwa ajili yao, na waamini wote.[8] Angalia Yohana 14:2

.....

.....

.....

URITHI WA MILELE

Kwa nini kung'ang'ania tusichoweza kutunza?

Kila kitu katika ulimwengu huu kinapita, lakini Mbingu ni kitu cha pekee kitakachaodumu milele. Kifo cha Kristo na ufufuo vimeleta uridhi huu usioisha kwa kila muumini. Soma 1 Petro 1:3-4. Andika mstari 4

.....

.....

.....

NA MWISHO

Kama kweli Yesu ni Mwana wa Mungu (angalia masomo yaliyotangulia), hivyo kufa kifo cha kusikitisha inashangaza, na inahitaji maelezo. Kwa uhakika, tumtegemee Mungu atupatie moja.



Upendo, siyo misumari, ulimjaa Yesu

Waandishi wa Agano Jipya wanaonekana kutupatia maelezo ya Mungu. Somo hili limekuwa ni maelezo yao kwa nini Yesu alikufa. Kama tutakubaliana kuwa wametupatia maelezo sahihi ya maisha Yake, kasha tutakiwa kuwa wazi kwa kile walichokisema juu ya *kusudi* la kifo Chake. Kwa hakika, ujumbe wa juu wa tabia ya Agano Jipya uliopendekezwa haukutolewa ili kutudanganya.

Kuna kitu cha ajabu juu ya kifo cha Yesu. Alipokuwa amening'inia msalabani Alipaza sauti yake akasema "Mungu Wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha".[9] Maelezo mazuri katika kilio hiki ni kwamba Mungu alikuwa anamwadhibu Yesu kwa ajili ya dhambi za wengine.[10]

Yesu kwa hiyari kabisa aliteseka kwa ajili ya waasi kama sisi. Hakuna aliyechukua maisha Yake kutoka Kwake.[11] Maisha ya milele Mbinguni yatakuwa mafupi sana kutoa sifa zote na kumwabudu ambako Kunamstahili. Upendo wa ajabu jinsi hii ni wa hiari. Unataka maisha yetu, mioyo yetu, na utu wetu wote!

[8] Angalia Yohana 17:20 na 24.

[9] Mathayo 27:46.

[10] Linganisha kifo cha Yesu na kile cha Stephen, Mkristo wa kwanza kunyongwa. Ni nini kinachoweza kutofautisha? (Matendo 6:15 na 7:55-56).

[11] Yohana 10:18